INTEGRATING CAPACITY & COMMUNITY ADVANCEMENT ORGANIZATION

MALALA FUND

ASOME PROJECT

ASOME
NEWSLETTER

ISSUE #4
JULY 2023

OF THE YOUTH BY THE YOUTH & FOR THE YOUTH

UKATILI

"Ukatili" ni neno linalo maanisha vitendo au tabia za uonevu, ukandamizaji na kudhulumu zenye kusababisha madhara, mateso, au unyanyasaji kwa watu au wanyama. Ukatili unaweza kujumuisha aina mbalimbali za vitendo viovu na visivyo haki. Aina za ukatili zinaweza kugawanywa katika makundi kadhaa.

Katika jarida hili tutajikita Zaidi katika kuongelea ukatili wa kijinsia kwa mazingira yanayotuzunguka na ambao unaweza kuhusishwa na mila na desturi katika jamii yetu. Pia, jarida hili litaweza kuchambua athari za ukatili wa kijinsia, namna ya kuzuia na kutokomeza ukatili na sheria zinazo simama kutokomeza ukatili kwa wanawake na Watoto.

Zaidi, jarida hili litachambua mifano ya aina mbalimbali za ukatili wakijinsia zinazo tokea / zilizowahi kutokea katika jamii. Baadhi ya vitendo vya ukatili ambavyo vimezungumuziwa katika jarida hili ni kama ukatili kupitia vyombo vya mitandaoni, kurubuni wasichana na wanawake (ubakaji), utumikishwaji wa watoto, kukosa huduma bora za uzazi, kumchapa mwanamke na kadhalika.

Vitendo vya ukatili ambavyo vinahusishwa na mila na desturi ni kama vile ukeketaji, ndoa za mapema, kunyima watoto wa kike fursa ya kwenda shule, kutosaidia wanawake kazi za nyumbani, kunyima wanawake fursa ya uongozi, desturi ya wajane au wanawake kuto rithi mali na kumpa majukumu mengi mjamzito

UKATILI WA KIJINSIA

MAANA YA UKATILI WA KIJINSIA

Ukatili wa kijinsia unamaanisha ni kitendo chochote anachofanyiwa mtu yeyote mwanaume au mwanamke kwa lengo la kumdhuru au kumuumiza kisaikolojia, kimwili , kiafya, au kiuchumi. Ukatili wa kijinsia unafanywa na mtu au kundi la watu na kusababisha mateso na maumivukinyume na matakwa ya mtu na inasababishwa na nguvu zisizo sawa kati wa wanawake na wanaume au mtu na kikundi cha watu, Na kitendo chochote cha unyanyasaji wa kijinsia ambacho husababisha, au kinaweza kusababisha madhara ya kimwili, kiakili,kiuchumi, kingono au kisaikolojia au mateso kwa mtu, ikiwa ni pamoja na kuambatana na vitisho vya vitendo kama maneno makali ya kuogopesha na kutishia maisha, kipigo, utekaji, na kulazimishwa au kunyimwa uhuru binafsi , iwe inatokea hadharani au katika maisha ya kibinafsi.

Tafiti nyingi zinaonyesha kwamba wanawake ndio wahanga wakuu wa ukatili wa kijinsia na ukatili hutokea sehemu zote mijini na vijijini. Ripoti ya hivi karibuni Desember 10, 2022 ya Tathmini ya Jinsia Tanzania 2022 inaonyesha kuwa asilimia 40 ya wanawake waliopo katikati ya umri wa miaka 15-49 wamefanyiwa ukatili wa kimwili. Ukatili kati ya wanandoa unaonekana kukithiri zaidi katika maeneo ya vijijini, ikiwa ni 52%, ukilinganisha na wastani wa 45% kwa mijini.10 Des 2022.

AINA ZA UKATILI WA KIJINSIA

UKATILI WA KIMWILI: Ni kitendo anachofanyiwa mtu kinachohusisha kuumizwa mwili na huweza kuonekana moja kwa moja kwenye mwili au mwathirika kuhisi maumivu bila watu wengine kutambua ila huweza kuonekana kwa vipimo vya kiafya. Mifano ya ukatili wa kimwili ni vipigo, shambulio la mwili, kuchomwa mwili na moto au kitu chenye ncha kali, kuumizwa kwa matumizi ya silaha, kuvutwa nywele, kusukumwa, kungatwa au ukatili wowote mwingine unao husisha mwili.

UKATILI WA KISAIKOLOJIA/ KIHISIA: Ni ukatili ambao mtu anatendewa au anakutana nao na unamsababishia maumivu kiakili na kihisia ambapo mtu mwingine hawezi kutambua kuwa mwenzake ametendewa utakili katika atua za awali hadi mazingira yatakapojitokeza na mtendewa akajieleza, lakini ukatili huu ukifanyika kwa wingi kwa mtu husababisha kukosa uelekeo, kushindwa kudhibiti hisia, kudhoofu kwa kushindwa kujichanganya na watu wengine na kuchanganyikiwa kiakili kwa kuanza kuzungumza mwenyewe kwasababu ya msongo wa Mawazo.

UKATILI KATIKA UHUSIANO: Ukatili huu huambatana na vitendo vinavyohusiana na masuala ya ngono. Mfano wa unyanyasaji/bugudha za kjinsia, ubakaji, ubakaji ndani ya ndoa, ulawiti, utekaji na usafirishaji wa wanaume au wanawake na watoto kwa ajili ya ngono, utumwa wa kingono, mashambulio yanayopelekea kuingiziwa vitu vigumu kwenye sehemu za siri.

UKATILI WA KIUCHUMI: Ni aina ya ukatili ambao unamnyima fursa za kiuchumi mwanamke au mwanaume katika kujiongezea kipato na kuchangia katika maendeleo. Aina hii ya ukatili inawakumba sana wanawake katika jamii nyingi wanawake wanakosa haki ya kujisiamamia kiuchumi na kumiliki mali. mfano wa ukatili huu ni kunyang'anywa mali, ubaguzi katika fursa za kiuchumi na kunyimwa haki ya kumiliki ardhi au mali, kunyimwa fursa za kujielimisha na vinginevyo.

UKATILI UNAOTOKANA NA TAMADUNI AU MILA POTOFU: Aina hii ya ukatili inachangiwa au unatokana na mila na desturi za jamii zinazo zunguka jamii husika ambazo zinaenda kinyume na haki za binadamu hivyo kuchangia kuwepo kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia. Kwa mfano, ndoa za kushurutisha, ndoa za utotoni, kurithi wajane, ukeketaji, kupiga wanawake kwa kuamini ndio upendo, ukeketeji, kuteka mabinti, miiko ya chakula, kunyimwa haki ya kumiliki ardhi, mali na ukatili utokanao na mahari.

UKATILI WA KIJINSIA KUPITIA MITANDAO YA KIJAMII. Ukatili wa kijinsia kupitia mitandao unakuwa siku hadi siku, kwa maeneo ya vijijini bado haujajulikana vema kwa watu wengi. Ukatili huu huwakuta zaidi vijana wanaotumia vyombo vya habari vinavyohusisha mawasiliano ya kimtandao.
Ukatili wa kijinsia kwa njia ya mitandao unapotokea husababisha athari nyingi hasa za kisaikolojia. Mtu anayetendewa ukatili huu huwa na hofu, wasiwasi, hukosa amani, hukosa furaha na pia husononeka na kukosa kujiamini. Mara nyingine muathirika anaweza hata kujidhuru kutokana na hofu na fedhea anayo kumbana nayo. Mfano wa ukatili kupitia mitandao ya kijamii ni kumdhalilisha au kumtukana mtu kwenye mtandao, kumsema mtu kutokana na muonekano wake, hali yake ya kiafya au namna yeyote inayo umiza na kukosesha furaha na kutuma picha za faragha au vitendo vya faragha vinavyoashiria udhalilishaji.

UKATILI WA KIJINSIA KWA KUITELEKEZA FAMILIA. Kutelekeza familia ni ukatili wa kijinsia, na hufanywa hasa na wanaume. Tabia hii husababisha chuki, maradhi na watoto kukosa haki zao za msingi kama elimu, chakula, mavazi na kujikuta wanakuwa Watoto wa mtaani kwani Jukumu la malezi ya watoto ni la wazazi wote. Mfano wa ukatili huu ni kuiacha familia wakati wa mafanikio kama wakati wa mavuno, kupata kazi, na shughuli yeyote inayoleta neema na Kwenda kujihusisha na wanawake wengine ikiwa familia yake kaiacha inateseka.

UKATILI WA KURITHI MALI ZA MJANE NA KUTHITHISHWA MKE (MJANE). Desturi ya kurithi mali za marehemu na wajane ni ukatili wa kijinsia. Ukatili huu unaweza kusababisha umasikini katika familia husika, na kuchangia Watoto kukosa mahitaji ya muhimu kama chakula, mavazi malazi, elimu na uhakika wa matatizo. Hali kadhalika wajane hukata tamaa ya maisha, hujenga chuki, visasi, msongo wa mawazo na matatizo ya kisaikolojia. Tambua, mali za marehemu ni haki ya familia yake.

UKATILI WA KIJINSIA KWA WATOTO WA KIKE

UKATILI WA KUMNYIMA HAKI YA ELIMU MTOTO WA KIKE. Elimu ni haki ya mtoto wa kike na wa kiume. Kumyima elimu mtoto wa kike ni kumkosesha haki yake ya msingi. Hali ya mtoto wa kike kukosa elimu huchagiza mimba za utotoni, ndoa za utotoni, umasikini unaochochewa na utegemezi na ongezeko la unyanyasaji kwa watoto kike. Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 inaeleza kwamba ni jukumu la mzazi, mlezi au mtu yeyote anayeishi na mtoto kumpa haki ya elimu na kujifunza. Mpe mtoto wa kike elimu umkomboe na vitendo vya ukatili wa kijinsia. Mtoto wa kike akielimika jamii nzima inaelimika, Hakuna zawadi bora kwa mtoto kuliko elimu.

UKATILI WA KIJINSIA UNAO SABABISHWA NA VISHAWISHI NA ULAGHAI. Vishawishi na ulaghai kwa watoto wa kike ni ukatili wa kijinsia. Umbali wa kwenda shuleni kwa wanafunzi ni tatizo kubwa katika jamii yetu, hasa kwa watoto wa kike. Baadhi ya watoto hujikuta katika ushawishi na ulaghai hali inayosababisha kukata tamaa na kukatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupata mimba na kuolewa katika umri mdogo. Mfano wa vishawishi na ulaghai ni kutumia kigezo cha kumsaidia kwa kumpatia usafiri kwa lengo la kumbaka, kumlawiti, au kumshawishi kingono. Jamii inawajibu wa kutafakari na kuchukua hatua hasa kuongeza ulinzi kwa watoto. Wazazi wana wajibu wa kufuatilia mienendo ya watoto wao.

Ukatili wa kijinsia haukubaliki kwa namna yeyote ile katika jamii. ukatili wa kijinsia unakandamiza haki za msingi kwa mtu binafsi na unazuia maendeleo.

UKATILI WA KIJINSIA KUPITIA NDOA KATIKA UMRI MDOGO. Ndoa za utotoni ni ukatili wa kijinsia. Pia ndoa za utotoni ni ubakaji. ndoa za utotoni zina athari sana kwa wasichana kwa sababu ni chanzo kikuu kinachochangia/kinachowafanya wasichana kukosa elimu, matatizo ya kiafya wakati wa kujifungua yanayochangiwa na kutoka damu nyingi na kuchanika kwa sehemu za siri kwa sababu ya udogo wa maumbile, kuelemewa na majukumu, kukosa haki ya maamuzi, mimba za utotoni na hata tatizo la fistula. Usiruhusu mtoto wa kike kupoteza afya yake, fursa ya kupata elimu na kufurahia utoto wake kwa kumuingiza katika ndoa akiwa na umri mdogo.

Ukatili unapaswa kuripotiwa au kutolewa taarifa popote unapotendeka au unapo ashiria kutendekea. Ukatili wa namna tajwa apo juu au unaoshabihiana na aina yeyote ile, unatakiwa kutolewa taarifa kwa dawati la jinsia, kiongozi wa serikali, waalimu, vituo vya afya,wazazi na polisi kwa ajili ya kuchukua hatua za kisheria kwa yeyote aliye tenda ukatili.

SHERIA NA SERA ZINAZOHUSU UKATILI WA KIJINSIA KWA WATOTO WA KIKE

Msingi ya ukatili (GBV) ni hali halisi nzito katika maisha ya wanawake wengi nchini Tanzania. Inatokana na mitazamo ya kijinsia na upungufu wa usawa wa kijamii na kiuchumi ambao huwapa wanaume upendeleo kuliko wanawake. Kuna ufahamu unaozidi kuongezeka nchini Tanzania kuhusu ubaguzi wa kijinsia na ukosefu wa usawa wa kijinsia katika maeneo tofauti ya maisha. Uamsho huu unaambatana na kukubali kwa kiwango kikubwa jinsi GBV ilivyoenea na jinsi inavyosababisha madhara siyo tu kwa wanawake na wasichana, bali pia kwa wanaume na wavulana, na zaidi ya hayo, kwa uchumi na mfumo wa afya na ustawi wa jamii wa nchi Aidha, Bado kuna upenyo mkubwa katika Sheria na Sera za Tanzania katika swala la Ukatili Wa Kijinsia.

Sheria ya Makosa ya Kijinsia na Masharti Maalum" ya mwaka 1998. Imetoa adhabu kali kwa wahalifu wa ukatili wa kijinsioa kwa wanawake na watoto lakini ina upenyo sheria hii haizungumzii ubakaji katika ndoa (maritial rape). Aidha takwimu na data kuhusu ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa kingono bado ni haba kwa ujumla katika viwango vyote kwa sababu hakuna njia rasmi ya kukusanya data. Serikali hukusanya taarifa kuhusiana na utekelezaji wa SOSPA kutoka kwa mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau wengine. Ukosefu wa sheria inayolinda dhidi ya unyanyasaji wa ndani ya ndoa chini ya Sheria ya Ndoa pia haifanyi ubakaji wa ndoa kuwa kosa.

Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971

Sheria ya Ndoa inaweza kuchukua hatua kadhaa za kisheria kuhakikisha ulinzi na kuzuia ukatili wa kijinsia:

1. Umri wa Ndoa: Sheria inaweza kuweka umri wa chini wa ndoa ili kuhakikisha kwamba watoto wadogo hawalazimishwi kuolewa kinyume na mapenzi yao. Hii inalenga kuzuia ndoa za utotoni ambazo zinaweza kusababisha ukatili na unyanyasaji.

2. Kulinda dhidi ya Ndoa za Kulazimishwa: Sheria inaweza kuharamisha ndoa za kulazimishwa na kuanzisha taratibu za kuhalalisha ndoa ili kuhakikisha kwamba pande zote zinaridhia kuingia katika ndoa.

3. Kupinga Ukeketaji na Unyanyasaji wa Kijinsia: Sheria inaweza kuchukua hatua za kisheria kuzuia vitendo vya ukeketaji na unyanyasaji wa kijinsia, na kuhakikisha kuwa wale wanaotenda vitendo hivyo wanawajibishwa kisheria.

4. Kutoa Huduma za Kisheria na Ulinzi: Sheria inaweza kuanzisha mifumo ya kutoa huduma za kisheria na ulinzi kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na vituo vya ushauri nasaha na mahakama maalum za kushughulikia kesi za ukatili wa kijinsia.

5. Elimu na Uhamasishaji: Sheria inaweza kuhimiza elimu na uhamasishaji kuhusu haki za binadamu na ukatili wa kijinsia ili kuongeza uelewa katika jamii na kuhakikisha watu wanafahamu haki zao na jinsi ya kutoa taarifa kuhusu vitendo vya ukatili.

Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009

Sheria hii 2009 inalenga kulinda haki na ustawi wa watoto na kutoa ulinzi dhidi ya ukatili wa kijinsia. Baadhi ya vipengele ambavyo sheria hii inaweza kuzingatia kudhibiti ukatili wa kijinsia ni pamoja na:

1. Kulinda dhidi ya Ndoa za Utotoni: Sheria hii inaweza kutoa masharti ya kisheria yanayohusiana na umri wa ndoa ili kuhakikisha kuwa watoto wadogo hawahusishwi katika ndoa kinyume na mapenzi yao.

2. Kupinga Ukeketaji na Unyanyasaji wa Kijinsia: Sheria ya Mtoto inaweza kutoa vifungu vya kisheria vinavyoharamisha ukeketaji na vitendo vingine vya unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto, na kuweka adhabu kali kwa wale wanaotenda vitendo hivyo.

3. Huduma za Kisheria na Ulinzi: Sheria hii inaweza kuanzisha mfumo wa kutoa huduma za kisheria na ulinzi kwa watoto walioathiriwa na ukatili wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na vituo vya ushauri nasaha na njia za kuwasilisha malalamiko.

4. Elimu na Uhamasishaji: Sheria ya Mtoto inaweza kuweka mkazo katika kutoa elimu na uhamasishaji kuhusu haki za mtoto na jinsi ya kuzuia na kutambua ukatili wa kijinsia, ikihusisha wazazi, walezi, na jamii kwa ujumla.

5. Kuimarisha Mamlaka ya Mahakama: Sheria hii inaweza kutoa mamlaka kwa mahakama kusikiliza kesi za ukatili wa kijinsia kwa watoto na kuhakikisha kwamba haki inatendeka.

HITIMISHO

Ni muhimu kuelewa kuwa sheria peke yake haiwezi kutatua tatizo la ukatili wa kijinsia. Utekelezaji wa sheria, ushiriki wa jamii, na kuongeza ufahamu juu ya ukatili wa kijinsia ni muhimu katika kuleta mabadiliko ya kijamii na kuwalinda watoto dhidi ya ukatili. Pia, Elimu kuhusu masuala ya kijinsia, Jamii nyingi hazijapati elimu kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia. Viongozi wa jamii wana wajibu mkubwa wa kuielimisha jamii kuhusu sababu, aina na athari za ukatili wa kijinsia. Wanufaika wa elimu hii wanao mchango mkubwa katika kubadilisha mitazamo na matendo ya wanajamii wengine.

Kwa ushirikiano huo tunaweza kubadilisha mitazamo ya wanajamii kuhusu usawa wa kijinsia. Saidia kuwaelimisha ndugu, jamaa na marafiki kuhusu madhara yatokanayo na ukatili wa kijinsia.

INTEGRATING CAPACITY AND COMMUNITY
ADVANCEMENT ORGANIZATION

P.O Box 31261 Dar es Salaam
Plot No 43 KJ Mwenge
0756 795022
e: info@iccao.or.tz
w: www.iccao.or.tz
iccao_tanzania